TANGAZO LA SERIKALI NA. 322 la tarehe 25/08/2017

SHERIA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153 (1)

_____

SHERIA NDOGO ZA (USAFI NA HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YAWILAYA YA ULANGA, ZA MWAKA 2017

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Usafi na Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Ardhi tengwa" maana yake ni sehemu ya ardhi ambayo imetengwa maalum kwa ajili hifadhi ya mazingira;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lililoundwa kwa mujibu kifungu la 16(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191;

SURA 191

4. "*Bioanuwai"* maana yake ni tofauti kati ya viumbe hai kutoka vyanzo vyote ikiwa ni pamoja na mifumoikolojia ya nchi kavu, mifumoikolojia ya majini na ikolojia changamani ambayo ni sehemu ya mifumoikolojia hiyo;

"Chanzo cha maji" maana yake ni mahali popote ambapo maji yanapatikana katika uhalisia wake na panaweza kuwekwa miundombinu ya maji kwa ajili ya matumizi ya Binadamu na viumbe hai wengine;

"Elimu ya mazingira" maana yake ni elimu itakayohusu mchakato wa kutambua sifa na kufafanua dhana ya mazingira ili kuboresha taaluma na mtizamo muhimu kwa ajili ya kuelewa na kukubali uhusiano kati ya binadamu, utamaduni na hali hai inayomzunguka;

"Eneo la Hifadhi'' ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga;

"Hifadhi ya Mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na afisa mwidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yeyote.

"Kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu, harufu mbaya na kuudhi, kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile nzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au aviumbe wengine hatari, mlipuko wa magonjwa au kusababisha madhara ya afya kwa binadamu, na viumbe

"*Madini ya Ujenzi"* maana yake ni Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi.

"*Mazingira*" maana yake maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabianchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe, hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

"Mfumoikolojia" maana yake ni elimumwendo changamani ya jamii za mimea, wanyama, vijiumbe na mazingira yao vikiwemo vitu visivyo hai;

"Mkaguzi wa Mazingira" maana yake ni Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya mazingira kwa jina au kwa wadhifa kuwa mkaguzi wa mazingira kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

*"Mkurugenzi"*maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga au Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri

"Mifugo" maana yake ni ng'ombe, punda, kondoo, mbuzi, nguruwe, mbwa na mifugo mingine ifugwao na binadamu;

"Taka" maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira.

"Taka gesi" maana yake ni hewa chafu, moshi, joto, au harufu ambayo inaweza kuleta madhara kwa Binadamu, mazingira, na viumbe hai wengine;

"Taka Ngumu" itahusisha taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps);

"Taka yenye madhara" maana yake ni kitu chochote kigumu, majimaji, cha gesi au taka majimaji ambayo kwa sababu ya athari zake kikemikali, athari kwa mazingira na binadamu, maambukizo yake, kiwango chake cha sumu, ulipukaji na kulika/kubabuka kwake kinadhuru afya, maisha ya binadamu au mazingira;

"Taka vimiminika" maana yake ni taka zilizo katika hali ya maji au vimiminika vitokavyo majumbani, kwenye kilimo, maeneo ya biashara au viwandani vilivyofanyiwa au visivyofanyiwa usafishaji;

"Taka za viwanda" maana yake ni taka zitokanazo na viwanda vinavyozalisha au visivyozalisha, ambayo ni chanzo cha nishati, maji, mitambo ya kusafisha au mawasiliano pamoja na taka-ngumu zilizoelezwa chini ya Sehemu ya IX;

"*Tathmini ya Athari kwa Mazingira"* maana yake ni uchunguzi wa hatua kwa hatua unaofanywa kubaini iwapo programu, shughuli au mradi utakuwa na madhara kwenye mazingira;

"Uchafuzi wa mazingira" maana yake hali ya kusababisha mabadiliko hasi ya hali ya hewa, na uoto wa asili, au uwepo wa kelele au kero za aina yeyote, harufu mbaya, uwepo wa taka za aina yoyote, ambapo unasababisha hali ya hatari kwa afya binadamu na viumbe hai wengine;

"Ukaguzi wa mazingira" maana yake ni tathmini yenye lengo, utaratibu, kumbukumbu, inayofanyika vipindi maalumu kwa madhumini ya kufahamu ni kwa kiasi gani mpangilio wa kimazingira, usimamizi na maandalizi yanavyofanywa katika kuhifadhi na kulinda mazingira;

"*Uchafu Hatari*" Kama ilivyotafisiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira.

"*Udongo*" Kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni pamoja na dunia, mchanga, miamba, miamba tope, madini, uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi

"Waziri'' maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa

SEHEMU YA PILI
USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Haki ya kuwa na mazingira safi, salama na kiafya

5. Kila Mtu atakuwa na haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya.

Wajibu wa kulinda, kutunza na kuhifadhi mazingira

6. Itakuwa ni Wajibu wa kila Mtu, Taasisi au Asasi yoyote kulinda, kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kuhakikisha kwamba:-

(a) anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake;

(b) anafanya shughuli zisizoathiri au kusababisha uharibifu au uchafuzi wa mazingira;

(c) anashiriki katika jitihada mbalimbali za utunzaji, uhifadhi na uendelezaji wa mazingira;

(d) anatoa taarifa kwa Halmashauri au Mamlaka nyingine kuhusu uwepo wa shughuli yoyote inayoathiri au inayoweza kuathiri mazingira au uwepo wa viashiria vya uharibifu wa mazingira.

SEHEMU YA TATU
USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

7. Itakuwa ni wajibu wa kila Mtu, Taasisi au Asasi yeyote kufanya usafi na kutunza mazingira na kuhakikisha kwamba:-

(a) Mazingira yanayozunguka eneo lake la makazi au biashara yanakuwa safi wakati wote;

(b) Anaweka na kutumia chombo cha kukusanyia taka za aina zote;

(c) Anachangia gharama za uzoaji wa taka kwa mujibu wa viwamgo vilivyotajwa na Sheria Ndogo hizi.

Siku ya usafi wa mazingira

8. (1) Halmashauri itatenga siku maalum itakayojulikana kuwa ni siku ya usafi wa mazingira ambapo watu wote watashiriki katika kufanya usafi wa maeneo ya umma na makazi.

(2) Siku hii inaweza kutumika kama siku maalum ya kutoa elimu ya usafi na mazingira kwa umma na kutoa tuzo kwa Mtu yeyote, Taasisi au Asasi ambayo imeshiriki vyema katika usafi na utunzaji wa mazingira.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) hapo juu, kila mtu ataendelea kutekeleza wajibu wa kufanya usafi wa kila siku katika eneo lake.

Wajibu wa kujenga na kukitumia choo

9. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mmiliki au Mpangaji wa nyumba ya makazi au ya Biashara kuhakikisha kwamba nyumba ina choo safi, bora na madhubuti kinachotumika na Wakazi wa nyumba hiyo.

(2) Mmiliki wa Nyumba, Jengo au sehemu yoyote ambayo inatumika kama makazi, eneo la biashara au eneo linalokusanya watu kwa muda mrefu ambaye baada ya ukaguzi ikagundulika hana choo ataandikiwa na Halmashauri Ilani ya kujenga choo itakayoonyesha muda wa kutekeleza ilani hiyo.

Umbali wa kujenga choo

10. Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya binadamu.

Vyoo vya umma

11. Halmashauri inaweza kujenga au kumruhusu Mtu yeyote, vikundi vya watu au Taasisi kujenga au kuingia ubia katika kujenga na kumiliki vyoo vya Umma *(Public toilets)* katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo na vitakuwa vya kulipia.

Vyoo katika maeneo ya mikusanyiko ya Watu

12. Mtu yeyote, Kikundi, au Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu wengi kwa wakati mmoja au Mmiliki wa hoteli, mgahawa au kilabu cha pombe, kanisa, misikiti, au Mtu yeyote anayemiliki jengo linalotumiwa na watu wengi atatakiwa kujenga vyoo vitakavyotosheleza matumizi ya watu wote na vitakavyotofautisha matumizi kwa kuzingatia jinsi.

Maegesho na Matengenezo ya magari na mitambo

13. (1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika katika karakana, gereji au maeneo maalum yaliyoruhusiwa kwa kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2) Ni marufuku kwa Mtu yeyote kuegesha gari bovu, au kufanya matengenezo, au kuosha gari, pikipiki, au mtambo wowote kwenye eneo la Barabara, hifadhi ya Barabara, njia ya waenda kwa miguu, mtaa, maeneo ya wazi, kando ya mito au maziwa, au eneo lolote ambalo halikutengwa kwa shughuli za aina hizo.

Udhibiti wa wadudu waharibifu na waenezao magonjwa

14. (1) Kila Mmiliki wa nyumba au jengo lolote atahakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji yaliyotuama, maji machafu, takataka, au kitu kingine chochote kinachoweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara ya afya binadamu.

(2) Mtu yeyote atayetaka kupulizia dawa ya kuua wadudu *(Furmigation)* au wanyama waharibifu katika nyumba, jengo au mahali popote atalazimika kuomba kibali kwa Halmashauri.

Usafi wa machinjio na maduka ya nyama

15. (a) Halmashauri itafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika machinjio na kuhakikisha kuwa machinjio zimetengenzwa kwa kiambaza cha saruji, mifugo inachinjwa katika machinjio hizo, upatikanaji wa

huduma ya maji safi, na kumetengwa maeneo maalumu ya kukusanyia taka.

(b) Wahudumu wa bucha za nyama na samaki watatakiwa kufanya biashara katika bucha zilizo katika hali ya usafi na watatakiwa kuvaa nguo safi nyeupe na kufunika vichwa kwa kofia.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI WA TAKA

Usimamizi wa Taka

16. Halmashauri itaweka utaratibu maalumu utakaohusu ukusanyaji na utupaji wa taka ambapo itawajibika kutenga maeneo kukusanya taka, kutoa elimu ya uchambuzi wa aina za taka na kupanga viwango vya ushuru wa kuzoa taka.

Uchambuzi wa taka

17. (1) Taka zote zitachambuliwa na kukusanywa kulingana na makundi, aina ya taka na sehemu zinakotoka ili kutoa nafasi ya usimamizi, usafirishaji na utupaji wake.

(2) Uchambuzi wa taka utafanyika kwenye chanzo cha uzalishaji wa taka ambapo:-

(a) taka zilizo na madhara zitatunzwa kwenye chombo cha rangi nyekundu kilichowekwa alama ya *"Taka hatarishi";*

(b) Taka zilizo na ncha kali zitatunzwa au kuwekwa kwenye vyombo au mifuko ya kipekee na kuwekwa alama ya kutoa tahadhari *"Hatari usifungue";*

(c) Taka zote zinazoweza kuwa taka rejea zitachambuliwa na kuwekwa kwenye vyombo vitakavyoelekezwa na alama maalum ya *"Recyclable".*

Uhifadhi wa taka kutoka viwandani

18. (1) Halmashauri itaelekeza na kukagua viwanda kama vimetenga na kutumia maeneo maalum ya kukusanya taka ngumu zinazotokana na shughuli za viwandani ambayo yako katika hali ya usafi na yanalindwa dhidi ya wadudu, wanyama, na viumbe wanaokula mizoga.

(2) Viwanda vinavyozalisha taka vimiminika vitahakikisha kwamba taka vimiminika zinasafishwa ili zisiwe na madhara kwa mazingira na kwa afya na zinahifadhiwa katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka na taka tope kabla ya kusafirishwa kwenda kutupwa katika malambo au eneo maalum yaliyotengwa.

Marufuku ya kutiririsha taka vimiminika

19. Itakuwa ni marufuku kutitirisha au kuelekeza maji taka, taka vimiminika au maji ya mvua kutoka viwandani, majumbani, majengo mengine kwenda kwenye vyanzo vya maji, barabarani, uchochoro, mtoni, maeneo ya wazi au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.

Ukusanyaji na uzoaji wa taka katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu wengi

20. (1) Halmashauri itasimamia shughuli za ukusanyaji na uzoaji wa taka kutoka katika maeneo ya masoko, Asasi, maeneo ya biashara, na maeneo mengine yenye watu wengi ambapo taka zitakusanywa sehemu maalum na kuzolewa kulingana na aina ya taka husika.

(2) Shughuli za ukusanyaji na uzoaji wa taka zinaweza kufanywa na Halmashauri au wakala wake kwa kadri watakavyokubaliana.

Taka za Hospitali

21. Ukusanyaji na utupaji wa taka za hospitali na dawa zilizofikia ukomo wa matumizi utafanyika kutokana na taratibu zilizowekwa na Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya utoaji wa huduma za afya.

Udhibiti wa taka gesi

22. Halmashauri itadhibiti uzalishwaji wa taka gesi kwa:-

(a) kutenga maeneo maalum ya ujenzi wa viwanda vinavyozalisha taka gesi eneo lililopo mbali na Makazi ya watu;

(b) kutoa elimu ya ujenzi wa nyumba za makazi zenye nafasi wazi za kutosheleza kuingiza na kutoa hewa na kupiga marufuku matumizi ya samadi ndani ya nyumba kama nishati ya kupikia.

Wachuuzi wa miwa, matunda na mboga mboga

23. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mchuuzi wa miwa, matunda au mbogamboga kuhakikisha kuwa ana chombo maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya bidhaa zake.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kufanya biashara ya miwa, matunda au mbogamboga pembeni mwa barabara au katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Udhibiti wa Taka zinazozalishwa kutoka katika vyombo vya usafiri

24. (1) Magari au mabasi yote yanayobeba abiria:-

(b) yatapaswa kuweka vyombo maalum vya kutupia taka zinazozalishwa na kuwataarifu abiria matumizi ya vifaa hivyo;

(b) yatakusanya na kutupa taka katika eneo lililotengwa kwa ajili kukusanya na uzoaji wa taka katika vituo vya mabasi au kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halma-shauri.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote akiwa ndani ya gari au mabasi, au chombo chochote cha usafiri kutupa nje kitu chochote au taka.

Chukizo au kero

25. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka au kujenga kitu chochote kinachoweza kusababisha kero au kilicho katika hali ya uchafu ambacho kinaweza kusababisha:-

(a) Madhara kwa maisha ya Binadamu,

Wanyama au viumbe hai wengine;
(b) adha, kero, chukizo au kelele kwa watu wengine;
(c) magonjwa.

Ilani ya kuondoa kero

26. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwepo kwa eneo lenye kero ya aina yoyote atamtaka kwa Ilani maalum Mmiliki wa Eneo hili, Mpangaji, Mtumiaji au mtu yeyote aliyesababisha kero hiyo kuondoa kero hiyo ndani ya muda utakaoainishwa kwenye ilani;

(2) Endapo Halmashauri italazimika kuondoa kero hiyo, gharama za kuondoa kero zitalipwa na mtu yeyote ambaye ni mpangaji au msimamizi au mwangalizi wa eneo hilo kabla au baada ya kuondoa kero.

Utupaji wa taka nyinginezo

27. Wazalishaji wa taka zinazotokana na madawa ya mifugo na kilimo, kemikali, shughuli za kilimo, au aina nyingine yoyote ya taka watakusanya, watazoa na kutupa au kusafirisha taka hizo kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa na Halmashauri.

Huduma ya maeneo ya kutupa taka

28. (1) Halmashauri itatenga, itajenga na kuendesha maeneo makuu ya kutupa taka *(Sanitary Landfills),* maeneo ya kutunza taka kwa muda *(Transfer statations)* na vituo vya kukusanyia taka *(Collection Points)* kabla ya kusafirisha kwenda Dampo Kuu;

(2) Halmashauri inaweza kumpa Wakala au kuingia Ubia katika kujenga na kuendesha maeneo ya kutupia taka.

(3) Wamiliki au wapangaji au wakazi wa maeneo ya makazi na biashara watalipia ada ya ukusanyaji na uzoaji taka kwa mujibu wa viwango vitakavyowekwa na kutangazwa na Halmashauri.

Marufuku ya kutupa taka ovyo

29. (1) Ni marufuku:-

(a) Kwa Mtu yeyote, Kampuni, au Asasi

yoyote kuzalisha taka na kuzitupa katika maeneo yasiyotengwa kwa ajili ya kutupa taka;

(b) Kuteketeza taka kwa kuchoma moto, au kufukia ardhini bila kibali cha Halmashauri;

(c) Kutupa taka kwenye mifereji, mitaro, mito, barabara, au maeneo ya wazi;

(d) Kutiririsha maji taka na taka vimiminika kwenye mifereji, mitaro, mito, barabara, au maeneo ya Wazi;

(e) Kufanya biashara au maonyesho ya biashara yeyote au shughuli nyingine yeyote katika maeneo ya karibu au ndani au juu ya mifereji au mitaro ya maji, au katika maeneo ya kukusanyia taka, au kwenye Dampo;

(f) kufanya biashara, kuweka mabango au kufanya shughuli yeyote itakayozuia matumizi ya maeneo ya hifadhi ya barabara *(Service road).*

Zuio la kufanya shughuli katika madampo

30. Ni marufuku kwa Mtu yeyote, Kampuni au Taasisi au Kikundi kufanya shughuli yeyote katika maeneo yaliyotengwa kuwa Dampo isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa na Halmashauri.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA UFUGAJI NA KILIMO

Wajibu wa mfugaji

31. Ili kutunza na kuhifadhi mazingira, kila mfugaji atakuwa na wajibu wa-

(a) kufuga idadi ya mifugo Kama itakavyoamriwa na Halmashauri;

(b) kufuga na kulisha mifugo katika maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halma-

shauri;

(c) kupitisha mifugo katika njia *(stock routes)* zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(d) kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(e) kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na halmashauri;

(f) kupeleka mifugo katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;

(g) kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;

(h) kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;

(i) kuweka alama kwenye mifugo yake (Branding, ear tags) na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;

(j) kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyo hitajiwa na Halmashauri;

(k) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o.

Masharti ya mfugaji

32. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote:-

(a) kuchunga, kulisha, au kunywesha maji mifugo katika maeneo yasiyotengwa kwa ajili ya kulishia mifugo au katika mashamba;

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani au kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine

bila kibali kutoka kwa Halmashauri;

(c) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;

(d) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo.

Ufugaji mijini

33. (1) Kila mfugaji wa mifugo au ndege atawajibika kukusanya na kutupa taka zote zitokanazo na wanyama au ndege hao katika maeneo maalum ya kutupa taka.

(2) Mfugaji atawajibika kufuga idadi maalum ya wanyama atakayoelekezwa na Halmashauri, kuwa na eneo la kulisha kutunza wanyama hao, na kuhakikisha wanafungwa katika eneo la pamoja na si kuzurura ovyo.

(3) Mfugaji atawajibika kuchukua tahadhari zote muhimu ili kuondoa au kuzuia uwezekano kwa kusababisha kero kwa Wakaazi wengine wa eneo hilo.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

34. (1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo.

(2) mifugo au mfugo wowote utakaokamatwa kwa kuzurura ovyo utalipiwa faini kwa mujibu wa viwango vitakavyoelekezwa na Halmashauri na baada ya kulipa gharama hizo Mfugaji atarudishiwa mifugo au mfugo wake kwa masharti ya kutorudia kosa.

(3) endapo mwenye mifugo au mfugo atashindwa kulipa faini ndani ya siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa

na haki ya:-

(a) kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama;

(b) baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo;

(c) na endapo Mfugaji hataonekana ndani ya siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri.

(5) endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda wa siku kumi na nne (14) Halmashauri itarudisha fedha za mauzo ya mifugo hiyo.

(6) Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote endapo kutatokea kifo kwa mifugo au mfugo kwa sababu zilizo nje ya uwezo wake.

Ukaguzi wa mifugo

35. Halmashauri itafanya ukaguzi kwa kuingia katika nyumba, jengo au zizi lolote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba , jengo au zizi hilo.

Wajibu wa Halmashauri

36. (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya:-

(a) malisho kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri;

(b) njia maalumu ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi kutoka malishoni au Minadani.

(2) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo itakayoonesha idadi na aina ya mifugo.

Taratibu za kilimo

37. Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za

kilimo zitakavyotolewa na Halmashauri.

Kuotesha mimea mirefu katika maeneo ya makazi

38. Ni marufuku kwa mtu yeyote kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu isipokuwa miti katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa na Halmashauri.

Masharti kwa mkulima

39. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima katika miteremko, karibu au katika vyanzo vya maji au maeneo oevu yaliyotengwa, kandokando au kwenye kingo za mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalohatarisha au kuleta uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya kilimo kwa kufanya jambo jingine kinyume na kilimo.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalumu cha maandishi kutoka kwa Halmashauri.

(5) Muda utakaoruhusiwa kuchoma moto rafiki kwa mujibu wa chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4.00 asubuhi.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za Kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia Kilimo cha kuhamahama na kuhimiza Kilimo cha mzunguko (crops rotation).

Matumizi ya viuatilifu

40. Halmashauri kwa kushirikiana na mamlaka husika za udhibiti wa viuatilifu zitaelekeza matumizi sahihi ya viuatilifu hivyo, na kufanya ukaguzi ili kubaini viuatilifu ambavyo si rafiki kwa mazingira.

Uchimbaji wa madini ya ujenzi

41. (1) Halmashauri itatenga maeneo maalum kwa ajili ya machimbo ya madini ya ujenzi kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba madini ya ujenzi katika makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya mito, ndani ya mto, bwawa au katika maeneo yasiyoruhusiwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

Kibali cha ujenzi

42. (1) Mtu yeyote atakayetaka kufanya ujenzi au kubomoa jengo atalazimika kuomba kibali cha ujenzi au kubomoa jengo kutoka Halmashauri.

(2) Halmashauri itafanya tathimini ya athari kwa mazingira na jamii kabla ya kuidhinisha ujenzi au ubomoaji wa Jengo lolote ili kudhibiti madhara ya kimazingira.

SEHEMU YA SITA
USIMAMIZI WA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

43. Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji kwa kuweka mipaka, alama na mabango ya ilani ya kuzuia uharibifu au uchafuzi katika maeneo hayo.

kulinda eneo la hifadhi

44. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji Kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha Maji isipokuwa Halmashauri.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

45. (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote, Kiwanda, Taasisi, Shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito au mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemichemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha Maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama

au viumbe vingine vilivyo hai.

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

46. Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji kwa kuweka mipaka, alama na mabango ya ilani ya kuzuia uharibifu au uchafuzi katika maeneo hayo.

Kulinda eneo la hifadhi

47. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

Uchejuaji wa madini

48. Ni marufuku kufanya shughuli za uchenjuaji wa madini au kuweka kitu chochote chenye sumu karibu au ndani ya chanzo cha maji au katika mito au maeneo mengine yanayotumiwa na binadamu au viumbe hai wengine.

SEHEMU YA SABA
HIFADHI YA MISITU

Uhifadhi wa uoto wa asili

49. (1) Halmashauri za vijiji zitawajibika kutenga na kuyatunza maeneo maalum kwa ajili ya hifadhi za misitu, uoto wa asili na viumbe hai wengine.

(2) Endapo maeneo hayo yatakuwa yameharibiwa, Halmashauri za vijiji zitahakikisha kuwa zinayarudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Kuchoma au kusababisha moto

50. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika Misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, Kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya

hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo kabla ya kusababisha madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Kibali cha kuchoma moto rafiki

51. Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto rafiki atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kwa majirani anaopakana nao kabla ya kuchoma moto katika eneo analokusudia na ataweka njia za kuzuia moto.

Uvunaji wa misitu

52. (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali kwa Taifa.

Wachoma mkaa na Kuni

53. Watu wanaovuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa au kuni watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa na ukataji wa kuni;

Wajibu wa kupanda miti

54. (1) Kila Mtu, Taasisi na Asasi katika Halmashauri atawajibika:-

(a) kupanda na kutunza miti katika eneo lake kulingana na idadi itakayoelekezwa na Halmashauri;

(b) Kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki.

(2) Halmashauri inaweza kupanga na kuitangaza siku maalum ya kampeni ya kupanda miti.

Taratibu za kukata miti

55. Mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti kwa matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi au shughuli nyinginezo, atalazimika kupata kibali cha maandishi toka kwa Mtendaji wa Kijiji au kibali cha Afisa Maliasili wa Halmashauri au Wasaidizi wake kwa miti iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri.

SEHEMU YA NANE
MAKOSA NA ADHABU

Makosa

56. Mtu yeyote ambaye:-

(a) ataingiza katika eneo la Halmashauri au atasafirisha mifugo ndani au nje ya eneo la Halmashauri bila kibali;
(b) atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;
(c) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa;
(d) atashindwa kufanya usafi katika Nyumba, jengo au zizi analotumia kufugia mifugo au ndege;
(e) atakayekiuka masharti ya kilimo kwa kulima katika miteremko, vyanzo vya maji, kingo za mito na maziwa, kutumia viuatilifu visivyoruhusiwa kisheria, au atafanya shughuli za kilimo katika maeneo ya malisho ya mifugo au eneo jingine lolote lisiloruhusiwa;
(f) atachimba madini ya ujenzi madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa;
(g) atatupa taka kwenye mitaro, barabarani, hifadhi ya barabara, vichaka au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;
(h) bila kuwa na sababu ya msingi atashindwa kushiriki katika siku ya usafi na mazingira iliyopangwa na Halmashauri;

(i) kwa makusudi ataharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji;
(j) atachafua kwa namna yoyote au kuweka sumu, kemikali au madawa ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu na viumbe hai wengine katika vyanzo vya maji au miundombinu ya maji;
(k) atachoma au kusababisha moto, atasafisha shamba, atachoma takataka bila kibali;
(l) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali au;
(m) atakata mti au kung'oa visiki au kuchoma mkaa na kukata kuni au kubangua magome ya miti bila kibali katika maeneo ya hifadhi au eneo lolote lisiloruhusiwa bila kibali cha Halmshauri;
(n) atatupa taka ovyo, tiririsha maji machafu, kuosha magari au mitambo, au kufanya jambo jingine lolote linaloweza kusababisha kero, adha au chukizo kwa watu wengine au kuharibu mazingira;
(o) ataendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa;
(p) atamzuia afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake au;
(q) atakwenda kinyume na masharti ya sheria Ndogo hizi.

Adhabu

57. Mtu yeyote atakayetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

58. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji kwa hiari yake mwenyewe atakiri kosa kwa maandishi na

kukubali kulipa faini na kutekeleza wajibu wake wa kulipa ushuru.

———

JEDWALI LA KWANZA

———

(*Chini ya kifungu cha 7(c)*

———

(A) ADA YA KUZOA TAKA

Na.	Aina ya Biashara	Viwango
1.	Makazi (kaya)	3,000/=kwa mwezi
2.	Mgahawa	5,000/= kwa mwezi
3.	Nyumba ya kulala wageni	15,000/=kwa mwezi
4.	Hoteli	15,000/=kwa mwezi
5.	Zahanati (taka zisizo hatari)	5,000/= kwa mwezi
6.	Kituo cha Afya (taka zisizo hatari)	10,000/= kwa mwezi
7.	Hospitali	20,000/= kwa safari
8.	Kiwanda cha kuuza mbao	10,000/= kwa mwezi
9.	Fundi seremala wakubwa	5,000/= kwa mwezi
10.	Fundi chuma	10,000/= kwa mwezi
11.	Karakana	10,000/= kwa mwezi
12.	Kiwanda kidogo	30,000/= kwa mwezi
13.	Kiwanda kikubwa	50,000/= kwa mwezi
14.	Duka la jumla	15,000/= kwa mwezi
15.	Duka la rejareja/huduma	7,000/= kwa mwezi
16.	Shule za Awali, Msingi na sekondari	20,000/= kwa mwezi
17.	Kituo cha kutunzia watu wenye mahitaji maalum	10,000/= kwa mwezi
18.	Baa	20,000/= kwa mwezi
19.	Kumbi za Sherehe	15,000/= kwa mwezi
20.	Dobi mdogo	5,000/= kwa mwezi
21.	Fundi wa vifaa vya umeme	5,000/= kwa mwezi
22.	Fundi kushona kwa cherehani	3,000/= kwa mwezi
23.	Saluni	10,000/= kwa mwezi
24.	Kituo cha kuuza mafuta	30,000/= kwa mwezi
25.	Stoo	5,000/= kwa mwezi
26.	Ghala	15,000/= kwa mwezi
27.	Klabu ya pombe ya asili	2,000/= kwa mwezi
28.	Washona viatu	2,000/= kwa mwezi
29.	Stoo za mkaa	10,000/= kwa mwezi

30.	Mama lishe/Baba lishe	5,000/= kwa mwezi
31.	Vituo vya kuoshea magari	20,000/= kwa mwezi
32.	Aina nyingine ya biashara/huduma	Itapangwa na Halmashauri

(B). ADA YA KUZOA TAKA ZINAZOTOKANA NA UBOMOAJI WA MAJENGO NA MABAKI YA VIFAA VYA UJENZI

Na.	*Ujazo kwa Tani*	*Kiwango*
1.	Tani moja	20,000

(C) GHARAMA ZA UTUPAJI TAKA KWENYE JALALA KUU

Na.	*Kiasi cha Taka*	*Kiwango*
1.	Chini ya tani moja kwa safari	5,000/=
2.	Tani moja kwa safari	10,000/=

_____

JEDWALI LA PILI

_____

ILANI YA KUONDOA KERO

(Chini ya kifungu cha 27)

Ilani hii imetolewa kwa mujibu kifungu cha 27 cha Sheria Ndogo za Usafi na Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga Mwaka 2017.

SEHEMU ‘A’

Ndugu……..... wa Mtaa/Kijiji …… Kata ya……Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……mwezi……..mwaka…. katika nyumba yako ya Biashara/kuishi iliyopo eneo la……..kumekutwa chukizo/kero/uchafu kama ifuatavyo;

1) ……..
2) ……..

SEHEMU ‘B’

Kwa ILANI hii unaamriwa ndani ya muda wa siku saba (7) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza kwa kuondoa/ kurekebisha/ au kusafisha machukizo/ kero/ uchafu uliotajwa hapo juu; kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa.

IMETOLEWA NA;	IMEPOKELEWA NA;
Jina;…….	Jina;…….
Saini……	Saini…….....
Wadhifa……...	Wadhifa……..
Tarehe……..	Tarehe……...

*Futa lisilohusika

_____

JEDWALI LA TATU

_____

ILANI YA KUJENGA CHOO

_____

(Chini ya kifungu cha 9(2)

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 9 (2) cha Sheria Ndogo za (Usafi NA Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, za Mwaka 2017.

SEHEMU ‘A’

Ndugu…….....wa Mtaa/Kijiji……Kata ya……Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……mwezi……..mwaka….Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma ya …….. iliyopo katika eneo la ……katika Kitongoji/Mtaa*……. Kijiji cha……Kata ya…….
Imekutwa haina choo/ choo kimejaa/kimeharibika* hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo;

(1) ……
(2) ……

SEHEMU ‘B’

Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika sehemu ‘A’ ya Ilani hii,

SEHEMU ‘C’
Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe…….endepo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itakuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

……..
AFISA MWIDHINIWA

IMETOLEWA NA;	IMEPOKELEWA NA;
Jina;…….	Jina;…….
Saini……	Saini…….....
Wadhifa……...	Wadhifa……..
Tarehe……..	Tarehe……...

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, umebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga uliofanyika tarehe 29. 01.2016 na Mhuri huo ulibandikwa mbele ya:-

YUSUF D. SEMUGURUKA,
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga

FURAHA F. LILONGELI,
Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga

NAKUBALI

Dodoma,
13 Julai, 2017

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.),
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI